



Pata muhtasari wa AfyaYangu/HelsaMi

Skani kodi ya QR au soma zaidi kuitia HelsaMi.no

#### Maelezo kidogo kwako kuhusu HelsaMi ni nini:

##### HelsaMi ni nini?

- Kupitia App au mtandaoni unawaza kupata muhtasari/maelezo kwa ujumla yanayohusiana na afya yako na kuwa na mazungumzo au mawasiliano na mfumo wa huduma ya afya– kwa njia rahisi na ya usalama.

##### Naweza kutumia vipi HelsaMi?

- Muhtasari wa makubaliano ya muda ulopangiwa na daktari
- Kutazama maelezo ya afya na matokeo ya majaribio ya kiafya -
- Barua na ujumbe
- Mashauriano ya kiafya kwa kuitia njia ya video
- Na mengi zaidi

##### Jee ni lazima nitumie HelsaMi?

Hapana, ni kwa hiari kabisa/si lazima. Unaweza kutumia simu ama barua kwa njia ya posta kama awali.

##### Jee maelezo yangu ni salama katika HelsaMi?

- Ndio, unaweza kuingia mtandaoni kwa kutumia ID-porten/ kitambulisho cha kidigitali kama kwa njia nyinginezo za huduma za umma.

##### Nani anaweza kutumia HelsaMi?

- Wewe ambaye una miaka zaidi ya 16 na unahitaji msaada wa kiafya au huduma za kuuguzwa kutoka hospitali, manipaa ama mganga mkuu/daktari ambao wanatumia HelsaMi. Tazama muhtasari kuitia [www.helsami.no](http://www.helsami.no)
- Unaweza pia kupata ruhusa ya kusoma maelezo ya kiafya kama mlezi au kwa niaba ya watoto wako mwenyewe.

##### Kitu gani ninachowea kukipata kwenye HelsaMi ambacho hakipatikani Helsenorge?

- Katika HelsaMi unaweza kuona maelezo juu ya rikodi ya afya yako, kwa mfano muhtasari wa kila uendapo kumwona daktari, baada ya mashauriano, ukilazwa hospitali na mengi zaidi.
- Unapata fursa ya kuwa na mazungumzo na watu kadhaa unaowasiliana nao wa huduma ya afya.

Platfromu ya afya inamilikiwa na manipaa ya kati ya Norway na Helse-Midt Norge.  
Tafsiri katika lugha mbalimbali [www.helsami.no](http://www.helsami.no)



[www.helsami.no](http://www.helsami.no)

